

## **ULIMWENGU WA KANGA**

**Rayya Timammy & Amiri Swaleh**  
**University of Nairobi**

This paper explains the many uses of 'kanga' or 'leso' as a medium for passing on messages of various types in the day to day life of a Swahili person. The paper explains the shape of the kanga, the various uses and the different expressions ('names') which are either poetic idiomatic expressions or prose type. Most of the expressions touch on the themes of religion, weddings, general words of wisdom, caution and admonition, congratulatory messages, parents and their immeasurable love and care, among others.

Makala haya yanaeleza umuhimu wa vazi la kanga au leso kama njia ya kupitisha jumbe za ainaaina katika maisha ya Mswahili. Tumeleza umbo la kanga, matumizi yake anuwai na maneno ('majina') yake tofautitofauti ambayo huwa aidha ya kishairi au kinathari. Maneno na kauli hizo hurejelea jumbe za kidini, harusi, maneno ya kawaida ya hekima, tahadhari na kuonya, kupongeza, wazazi na mapenzi yao yasopimika na moyo wao wa kujali, kati ya maudhui mengine.

### **1. UTANGULIZI**

Ulimwengu wa kanga au leso ni ulimwengu wa uzuri, rangi za kupendeza, nakshi changamano, mavazi ya kusitiri na papo hapo kupitisha ujumbe fulani kupitia methali, misemo na misimu. Kanga ina matumizi anuwai ya jamii, ni ya mapambo katika sherehe mbalimbali za kijamii. Leso ni sehemu muhimu ya utamaduni wa Mswahili na Mwafrica kwa vile matumizi yake yamepanuka nje ya mwambao wa pwani zilikoanzia.

Leso au kanga ni kitambaa cha umbo la mstatili kilichotengenezwa kwa pamba chenye urefu wa mita moja unusu na upana wa mita moja na sentimita kumi na ambacho hutarajiwa kumfunika mvaaji kutokea kifuani hadi karibu na jicho la mguu (Yahya-Othman, 1997:137). Ijapokuwa siku hizi kuna nyingine ambazo ni kubwa zaidi na hujulikana kama leso za 'kuswalia' miongoni mwa Waswahili kwa sababu hutumika na wanawake kujifunga wakati wa kuswali. Kwa kawaida, leso huuzwa kwa gora/doti /mti au vipande viwili na huvutia zaidi zikitumiwa pamoja. Gora ya leso inaponunuliwa huwa imeunganishwa upande wa mapana. Mnunuzi halafu huikata vipande viwili upande wa mapana na kuzipindisha ili zisitoke au kuchanikachanika nyuzi.

Makala hii inaeleza kwa ufupi, historia ya leso, muundo wake, majina yake, matumizi yake anuwai na baadhi ya misemo maarufu inayoandikwa kwenye kanga na maana zake. Hatimaye tutahitimisha kwa kutaja maswala yaliyoibuka katika ufafanuzi wetu.

## 2. HISTORIA NA UMBO LA KANGA

Ijapokuwa kanga zinakuja na zipo katika mitindo mbalimbali zenye rangi mbili au tatu, kanga halisi ya Afrika Mashariki huwa na sehemu tatu. Sehemu ya kwanza huwa ni pindo ambalo huwa limeizunguka kanga au lesu yote. Sehemu ya pili huwa ni ile sehemu iliyomo ndani ya pindo ambayo hujulikana kama mji, na sehemu ya tatu ni jina la kanga au ujumbe ulioandikwa (Yahya-Othman 1997:137).

Lesu zinaaminika zilianzia katika maeneo ya mwambao wa pwani katikati ya karne ya kumi na tisa. Kuna mawazo yanayohitilafiana kuhusu eneo hasa katika mwambao wa pwani ambapo vazi hili lilianzia. Jeannette Hanby na David Bygott (1985:1) wanasema wanawake wapambe wa Kizanzibar ndio walianzisha vazi la kanga walipokuwa wakiunga pamoja hankachifu sita ili ziwe kipande kikubwa cha kitambaa. Jeannette Hanby na David Bygott (1985:2) wanaendelea kusema mtindo huu mpya wa kitambaa ukaitwa 'lesu' kutokana na jina la hankachifu hizo zilizoletwa upwa wa Afrika Mashariki na Wareno na ambao waliziita 'lenco' kwa Kireno. Jina 'lesu' ni mojawapo wa maneno yaliyokopwa kutoka katika lugha ya Kireno. Naye mwanahabari wa Australia Troughhear, aliyeishi na kufanya kazi nchini Kenya anasema Charles New (1873:58), anaelezea kuwa, mtindo wa vazi hili ulianzishwa na wanawake wa Mombasa. Tunaelekea kukubaliana naye kwani jina 'lesu'ndilo hutumika nchini Kenya ilhali nchini Tanzania, jina linalotumika zaidi ni kanga. Jina lenyewe 'kanga' linaaminika kuwa lilianza kutumika mwishoni mwa miaka ya 1800 wakati wanawake wa Zanzibar walipozibandika jina 'kanga'kutokana na mtindo wa lesu zilizokuwa na vitonetone vyeupe na mwili mweusi kama yule ndege kanga katika lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, kuibuka jina la pili 'kanga', kukalipa vazi hili majina haya mawili yanayotumika kama visawe. Ijapokuwa, nchini Kenya jina lililoshika zaidi ni 'lesu' na jina linalotumika zaidi nchini Tanzania ni 'kanga'.

## 3. MANENO KATIKA KANGA

Mwanzoni kanga au lesu hazikuwa na maneno - yaani, misemo na methali au misimu. Inaaminika kuwa Abdalla Kaderdina ndiye alianzisha mtindo huu wa maneno kwenye lesu mwanzoni mwa miaka ya 1920 (Parkin, David 2004:1). Maneno yenyewe - ijapokuwa yalikuwa ya lugha ya Kiswahili, yaliandikwa kwa hati ya Kiarabu. Mwishoni mwa miaka ya hamsini ndipo hati za Kilatini zilitumika wakati matumizi ya lesu yalipopanuka kutoka kwa watu wa pwani na kuenea kote Afrika Mashariki.

Kulingana na Kaderdina Hajee Essak (*Swahili Language and Culture-internet*), watengenezaji na wauzaji wa kanga wanapata ilhamu ya maneno/misemo kutokana na misemo ya zamani ya Kiswahili, methali na hali za kisasa za siku kwa siku za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Wanatunga misemo

mingi wenyewe lakini wanapata chagizo na changamoto kutoka kwa wanajamii ambao ni wateja wao. Kwa kawaida, watu huwapelekea maneno na ikiwa yatachaguliwa kutumiwa katika lesu, basi huwa wanazawadiwa (Parkin, 2004:4) lakini wana watu wao maalum ambao ni wazee wanaowabunia maneno hayo. Maneno mengine hutolewa kutokana na kibwagizo au sehemu nyingine za nyimbo za taarab zilizotia fora katika vipindi fulani. Kwa mfano, msemu kama ‘Wape wape vidonge vyao’ lilitokana na wimbo wa mwimbaji taarab ajulikanae kama Aisha Abdulwahab (Malika) katika miaka ya tisini au kauli kama ‘Yailahi nipe moyo wa subira’ kutokana na wimbo wa Marehemu Ustadh Juma Bhalo katika miaka ya sabini.

Nyongeza hii ya maneno kwenye lesu imeziwezesha kuwa fasiri na jukwaa la kutolea kauli za jamii kama ilivyo historia ya Afrika Mashariki. Karibu lesu zote huwa na maneno isipokuwa chache ambazo husemekana au huitwa lesu “bubu” yaani, hazisemi kwani lesu husemekana kuwa “zinasema na kusemezana”. Misemo hii kwenye kanga mara nyingi huwa haiko wazi au haieleweki kwa uwazi au huwa tata - yaani usemi mmoja unaweza kufasiriwa kwa njia kadhaa kutegemea mtumizi na mara nyingine hata eneo la kijiografia inakovaliwa lesu hiyo.

Mara nyingine misemo hii ni ya kishairi (na huwa na wizani na midundo). Ndipo misemo yenyewe ikawa inatumia sitiari na tashbihi kusawiri picha mbalimbali za maisha ya Uswahilini na maumbile yake na kwingineko. Kwa mfano, msemu ‘Mchafuko wa bahari si mwisho wa safari’, unaweza kufasiriwa katika muktadha wa maisha kwa jumla au hata vipengele tofautitofauti kama panda-shuka za maisha ya ndoa.

Kama methali za Kiswahili ambazo hutungwa aidha kishairi au kinathari, majina hayo yanaweza kuwa na vina au mdundo au yote mawili (Tazama Knappert 1967, anapozungumzia muundo wa tungo za kimapokeo za kishairi). Wanawake wa pwani (na hapa hasa tunawarejelea wa Kiswahili na Kidigo), hununua kanga kwa wingi (na hata kuna msemu kuwa “mwanamke hafurahi mpaka apate kanga elfu”), huitazama misemo hii kama jumbe maalum. Utumizi wa lesu humruhusu mvaaji au mtoaaji lesu hizo kutuma jumbe ambazo ni ngumu kuzipitisha au wanaona ugumu kuzieleza kwa maneno. Kwa mfano, mtu anapotambua kuwa mtu aliyedhani ni rafiki amemsaliti au kumweleza mama-mkwe, wafi na hata mume k.m. ‘Tulia tuishi wazuri haweshi’, ‘Ya nini kunibwagia koko na embe kumpa yeye’, ‘Semeni mnayojua msikae mkizua’, ‘Hunilishi hunivishi na hunibabaishi’, ‘Penzi ni vitendo sio maneno’, n.k. Ijapokuwa mara nyingine jumbe huwa si ngumu kueleweka, hutokea baadhi ya misemo ikawa tata na changamano. Kwa kweli katika muktadha huu wa jumbe ambazo ni wazi au rahisi kueleweka, lesu hutumika kama kadi za salamu, za kumtakia mtu afueni kutokana na maradhi au kumpongeza au kupeana au kutoa mkono wa tahania katika utamaduni wa Kimagharibi, ijapokuwa katika muktadha huu, ujumbe huwa na maana zaidi ya ile ya kawaida (Beck 2001:157).

Kuna kanga inayofaa kwa kila tukio au hali. Kanga zinaweza kuonyesha hisia za mapenzi, kutoridhishwa na jambo au hali fulani, kutoa au kuonyesha shukrani, upendezwaji na jambo au hali fulani, majuto, na karibu hisia nyingine yoyote ya kibinadamu. La kufanya ni kuchagua tu kanga iliyo na ujumbe mwafaka. Na ndiyo sababu wake na hata waume wanaponunuliana kanga, hawaangalii rangi, uzuri au nakshi tu za lesu bali wanaangalia au kuvutiwa na jumbe za maandishi au majina yake. (Kanga zenye jumbe za matusi au za kuudhi au zenye mafumbo hazitolewi kama zawadi - ndipo ikazungumziwa kuhusu kuvaa kanga na wala sio jina lake). Waume huwapa wake zao kanga kuonyesha urafiki au mapenzi au hata kuchukizwa na jambo fulani. Misemo mingi hutoa busara ya kilimwengu, huelimisha, hutoa falsafa au mwonoulimwengu wa Waswahili na ushauri kuhusu tabia njema na maadili kwa ujumla (Tazama Timammy na Swaleh (2013) wanavyozungumzia swala la maadili katika jamii ya Waswahili). Misemo hii imesiisitizwa sana katika utamaduni wa Waswahili sawa na jamii nyingine za Kiafrika.

Hanby na Bygott (1985) wanaeleza matumizi mia moja na moja ya lesu. Miongoni mwa Waswahili wenyewe, lesu hutumika kama nguo za kulalia kati ya mke na mume chumbani mwao na ndipo zikawa ni vipande viwili ijapokuwa, mwanamume hatarajiwi kuonekana na watu wengine akiwa amejifunga kanga. Hivyo matumizi yake kwa mume ni chumbani pekee. Lesu zinatumiwa kama kibobwe kufanyia kazi nyumbani, kama tauli na pia kama nguo za kushindia nyumbani. Kitamaduni, lesu hupatiwa msichana kufunika kifua pindi kinapoanza kuinua nguo. Kanga hutumika kama matambara ya kupangusia, kukungutia na kupigia deki zinapokuwa kuukuu. Lesu pia hutumika kama njia ya mawasiliano, haya yakiwa baadhi tu ya matumizi yake. Kanga zinatumiwa na makundi au matabaka mbalimbali ya kijamii - wazee wa kike katika maeneo ya mashambani, wafanyikazi nyumbani, wanawake wa mijini, watoto wa shule katika tamasha za muziki na densi, waigizaji majukwaani na vikundi vya kina mama vya ngoma za kitamaduni na wengineo.

Katika wasilisho hili tunajihusisha na mojawapo tu ya matumizi yake - kama njia ya kujieleza au kuwasiliana au kupitisha ujumbe kupitia methali, misemo na misimu inayoandikwa kwenye lesu au kanga zenyewe. Zinapotandikwa vizuri kitandani zikiwa zimefukizwa udi vizuri, mume wa nyumba huwa anawasilishiwa ujumbe kuwa siku ile mkewe anataraji itakuwa siku yao kukutana. Lesu nyekundu zinapowekwa kitandani, zinaashiria kuwa yule mke si 'safi' yaani, ana hedhi na kwa hivyo, inapitisha ujumbe kuwa hawawezi kukutana. Lesu zinapofungwa juu ya jeneza (kwa Waswahili) hufahamisha kuwa aliyefariki ni mwanamke. Kwingineko bara, kama miongoni mwa jamii ya Wakikuyu, kanga ni vazi ambalo huitishwa na wazazi au jamaa za bibi harusi wakati wa kuposa. Hatimaye siku ya harusi yenyewe hutumika kufungia kibobwe na wanawake wanaosaidia kazi, na pia Bwana na Bibi Harusi hutandikiwa kanga hizo ili ziwe kama zulia la heshima kwa ajili yao.

Miongoni mwa jamii nyingine, kanga huvaliwa sare na kina mama wanapokuwa wakitayarisha chakula siku za harusi.

#### **4. MANENO YA MISEMO MAARUFU YA KANGA/LESO**

##### **4.1 Misemo ya mapenzi**

Baadhi ya misemo maarufu inayohusu mapenzi na ambayo inajitokeza katika lesu ni:

- Nimepata la Azizi dawa ya roho yangu
- Takuenzi uwe wangu maishani
- Nakupenda wewe sina mwengine
- Nilikuota wewe
- Si mzizi si hirizi bali moyo umeridhi
- Pendo likipata mjuzi humea mizizi
- Mahaba yetu asali hayahitaji sukari
- Mapenzi ya kweli kuishi wawili
- Kwako mtu hanitoi
- Pendo letu limoyoni
- Moyoni upeke yako
- Penzi halichagui rangi

##### **4.2 Ushauri kuhusu tabia njema**

Ushauri au nasaha ni kati ya mambo yanayohimizwa na kukokotezwa sio tu miongoni mwa jamii ya Waswahili bali jamii zote za binadamu kote ulimwenguni:

- Tabia njema humpamba mja
- Tabia njema thawabu kuliko dhahabu
- Tabia njema twabibu

##### **4.3 Misemo ya kidini**

Akali ya Waswahili ni waumini wa dini ya Kiislamu na ndipo tukaona jumbe nyingi zikielemea mafundisho na imani ya Uislamu :

- Yailahi nipe moyo wa subira
- Mola twashukuru
- Alitakalo Karimu haliwezi mwanadamu
- Mungu tupe imani tupendane duniani
- Kilichonyoshwa na Mungu kiumbe hakipeti
- Mungu ni mwema
- Kila muomba Mungu hakosi kujibiwa
- Dua ni dawa

#### 4.4 Jumbe za harusi

Familia ni kiungo na chemchemi muhimu ya binadamu. Hii ndio sababu Waswahili sawa na jamii nyinginezo za binadamu wakatilia mkazo sana asasi hii muhimu jambo linalojitokeza katika baadhi ya jumbe za kanga:

- Tamu ya harusi ni furaha
- Unipende kwa raha na shida
- Iwe harusi ya heri
- Tuishi kwa kupendana
- Raha ya ndoa ni kuvumiliana
- Yarabi ijaalie baraka harusi yetu
- Pendo letu liwe imara tuzidi kuelewana
- Kweli pendo likiwepo maisha huwa muruwa

#### 4.5 Misemo ya kijumla ya busara ya kilimwengu

Ipo misemo ambayo ni ya kijumla na yaweza kuafiki hali za jamii mbalimbali ulimwenguni na wala sio jamii ya Waswahili na mazingira yao pekee:

- Kauli njema yashinda utajiri
- Faida ya kujuana ihsani kutendana
- Kusubiri usichoke mazito huwa mepesi
- Nia njema ni tabibu
- Mapenzi hukuzwa kwa imani na huruma
- Ulimwengu bahari kiumbe jihadhari
- Muacha mila ni mtumwa
- Jirani ni dhahabu husaidia wakati wa tabu

#### 4.6 Misemo ya tahadhari/uangalifu

Kila jamii hutoa hadhari kwa wanajamii wake ili wawe na hadhari au wawe waangalifu katika harakati zao za maisha ya kila siku:

- Ya dunia hayataki pupa
- Mteka kilema hana mwisho mwema
- Muogope fisadi kiwembe
- Kuringa kwa mali ya mume ni kusumbua roho yako
- Dunia ni mapito dunia si yetu
- Mchezea jema baya humfika

#### 4.7 Kusherehekea sikukuu za Idd

Jamii ya Waswahili husherehekea sikukuu mbili muhimu ambazo ni Idd-ul-Fitri (baada ya mfuno wa mwezi mtukufu wa Ramadhani), Idul-Adh'ha (tarehe kumi ya mwezi wa Dhul Hijja baada ya hija):

201 Ulimwengu wa kanga

- Zawadi ya Idi Kusameheana
- Eid Mzaa Chema Idd Mubarak
- Eid Mubarak
- Zawadi ya Idd

#### **4.8 Misemo ya kupigana vijembe/kukejeli**

- Mgonjwa hupewa dawa mmbeya hupewa nini?
- Usione nacheka moyoni nakereka
- Heri kukatwa na bati kuliko kukosa bahati
- Tutakula nao wenye waume zao
- Maneno si mkuki msemayo si shituki
- Mkeka mkalie hata mkinitukana wifi yenu ndie mie
- Utatembea bucha zote nyama ni ile ile
- Isikuhadae rangi tamu ya chai sukari

#### **4.9 Misemo kuhusu umuhimu wa mama/wazazi**

- Asante mama kwa radhi yako
- Mama ni mama hakuna kama mama
- Usia wa mama ni muongozo duniani
- Mama ni malkia thamani yake peke
- Nani kama mama
- Mzazi ni mzazi
- Wema wa wazazi hauna mfano

Kuna pia kanga zinazosherehekea matukio ya kisiasa na kijamii ijapokuwa hizi zaidi hutengenezwa nchini Tanzania. Masuala ya kitaifa na sera zake pia hutetewa na kupigiwa debe kupitia lesu kama kampeni za upangaji uzazi na utambuzi wa magonjwa kama ukimwi. Nchini Kenya kwa mfano, kulikuwa na toleo maalum la lesu kusherehekea Mwongo wa Umoja wa Mataifa wa Wanawake mnamo mwaka 1985. Awamu ya Tatu ya Michezo ya Bara la Afrika ya mwaka 1997 na Ziara ya Papa nchini Kenya miaka ya 2000 ni matukio yaliyoadhimishwa kwa matoleo maalum ya kanga. Vilevile kumeshuhudiwa kanga maalum kwa ajili ya kampeni za chaguzi kuu zikisifu vyama vya kisiasa kwa mfano, kanga zilizotolewa na muungano wa Rainbow Alliance mnamo mwaka 2002 na wacombeaji wa urais, ubunge na udiwani. Mfano mzuri ni msemu 'Sina siri nina jibu' (katika kampeni za ubunge mjini Mombasa Najib Balala alipokuwa anawania kiti cha ubunge cha Mvita na Shariff Nassir).

### **5. FAFANUZI ZA BAADHI YA MANENO AU MAJINA YA KANGA**

Sehemuhii inachambua kauli au jumbe chache za kanga au lesu.

**(a) Bahati ni Upepo sasa Upo Kwangu**

Msemo huu unarejelea hali ya kwamba, hakuna binadamu anayeweza kudai kabahatika zaidi ya wengine; leo bahati huwa kwa fulani, kesho kwa mwingine sawa na jinsi upepo unavyovuma mara huku mara kule pasina uwezo au jitihada zozote za viumbe ulimwenguni. Pia hutumika kuonyesha kuwa mtu fulani ni rafiki ya mwingine au mume wa mtu fulani sasa yuko kwa mke mwingine. Aidha, msemo huu ni sitiari inayolinganisha bahati na upepo.

**(b) Ulimwengu Bahari Kiumbe Jihadhari**

Msemo huu unatumia kunga ya sitiari kuulinganisha ulimwengu na bahari. Kwa mtu anayeifahamu fika bahari, basi anajua kwamba, hali ya bahari haitabiriki; mara shwari, mara inachafuka na hata mabaharia na wavuvi stadi huiambaa kwa kuhofia usalama wao. Na ulimwengu nao, ndivyo ulivyo; mara mambo mazuri, mara yanabadilika ghafla na hali ya mtu ikawa mbaya au nzuri kuliko ilivyokuwa hapo awali.

**(c) La Tamu halina Siri**

Msemo huu una maana kuwa pindi linapotukia jambo jema, zuri au lenye faida iwe kwa mtu binafsi au kwa jamii, basi huwa halifichwi au halifichiki. Kinyume chake jambo la aibu au hizaya, aghalabu hufichwa ili lisetiri heshima ya mwanajamii mhusika au hata jamii au nchi husika.

**(d) Shingo huvaa Chombo Moyo huvaa Mambo.**

Msemo huu unarejelea hulka au tabia ya mwili na moyo wa binadamu kiulinganishi. Mwili wa mwanadamu hupambwa kwa mavazi ya ainaaina wakati moyo wake hupambwa kwa ridhaa au mambo mema. Msemo huu una maana kwamba, lazima mtu ajue kinachoufaa moyo na cha mwili. Vinginevyo, ni msemo unaohimiza uwastanishaji wa mambo maishani ndipo mwafaka upatikane. Mwanadamu anapopatwa na jambo lolote huwa lipo moyoni na mwanadamu mwingine anaweza asijue jambo hilo lakini chombo kinapovalwa huonekana na watu.

**(e) Shaba Kutu Maumbile**

Maumbile au kawaida ya vyombo vilivyoundwa kutokana na madini ya shaba huingia 'kutu' au hupoteza ule mng'aro wake asilia. Hii ina maana kwamba, lazima mtu aishi akijua na kutambua kila kitu kina kawaida yake na wala pasije pakaingia kutofahamikiana kutokana na mtu kutofahamu sifa halisi za kitu fulani. Kwa maana ya ndani pia unaweza kufasiriwa kuwa mtu mwenye tabia fulani iwe nzuri au mbaya ni sifa yake. Lakini kwa kuwa kutu ni ila hapa, inarejelea kuwa mwenye tabia mbaya ndio wasifu wake na hata akijaribu kubadilika anarejelea tabia ileile.



## 6. HITIMISHO

Tumefafanua vazi la kanga au lesu na umuhimu wake kama jukwaa la jumbe au maudhui mbalimbali miongoni mwa Waswahili. Japo lesu ilianza hankachifu zilizotokea ugenini zikaunganishwa, Waswahili wameifanya kanga jukwaa muhimu la kupashana habari na kuendeleza fasihi simulizi na hasa utanzu banifu au wa semi. Hii ndiyo sababu kanga au lesu kuwa na jumbe au maudhui anuwai na zenye umbo la kishairi na nyingine za kinathari. Kanga au lesu zina jumbe za mapenzi, wasifu, kejeli, za kutakiana heri ya sikukuu mbalimbali, busara za kilimwengu, kuwasifia na kuwaenzi wazazi kati ya nyingine. Tumechanganua maneno machache ya kanga na tukaona kuwa yana uzito wa kimaudhui zaidi ya kuwa ni maneno tu ya kanga.

## MAREJELEO

- Beck, R. 2001. "Ambiguous Signs: The Role of the *Kanga* as a Medium of Communication." *AAP Swahili Forum*, pp.157 - 169.
- Hanby, J. & D. Bygott. 1985. *Kangas: 101 Uses*. Nairobi: Hanby and Bygott.
- Knappert, J. 1967. *Four Centuries of Swahili Verse*. Leiden : E.J. Brill.
- Parkin, D. 2004. "Textiles as Commodity, Dress as Text : Swahili *Kanga* and Women's statements." Katika R. Barnes. *Textiles in Indian Ocean Communities*. London/New York: Routledge.
- Timammy, R. & A. Swaleh. 2013. "A Thematic analysis of *Utendi waMwanakupona*: A Swahili / Islamic Perspective." *Journal of Education and Practice*, Vol. 4 No. 28, 2013, pp. 8 -15.
- Yahya-Othman, S. 1997. "If the Cap fits: Kanga names and Women's Vice in Swahili Society." *Afrikanitische Arbertspapiere* No. 51, pp. 135-149.  
[http://www.glcom/Hassan/kanga\\_history.html](http://www.glcom/Hassan/kanga_history.html). 16.2.2015.4pgs  
<http://www.glcom.com/hassan/kanga.html>. 2.5.2015.9 pgs.

### *Authors' addresses*

Rayya Timammy  
E-mail: [rayyat@yahoo.com](mailto:rayyat@yahoo.com)

and

Amiri Swaleh  
Department of Kiswahili, University of Nairobi  
P.O. Box 30197 - 00100  
Nairobi, Kenya  
E-mail: [babake84@gmail.com](mailto:babake84@gmail.com)